# UPAKAJI RANGI KWA URAHISI

Goldstar PAINTS



Rangi Inayodumu Zaidi

## KWA NINI UPAKE RANGI:

Watu wengi walikua wakijiuliza "kwa nini wapake rangi"? Jibu ni rahisi sana,kwa sababu faida nyingi unazozipata zitajionyesha baadae.Kwanza unalinda kile ulichoamua kukipaka rangi,iwe ukuta wa nyumba yako,kabati,milango,viti,meza,uzio,au chochote unachokimiliki.Hii ina maana kwamba,unaongeza zaidi maisha ya mali yako. Kwa maisha ya sasa hiyo ni muhimu kwasababu gharama mnazolipia ni kubwa kwa kile mnachokinunua.Utakuwa mwenye busara kwa kuthamini kila unachokinunua.Kupaka rangi kutakusaidia kufanya hivyo.

Pili,unaweza kufanya kile unachopaka rangi kionekane kipya tena.Unaweza kujivunia nyumba yako na kile kilichomo ndani yake. Rafiki yako na majirani watashangazwa nawe,na wanaweza kuwa na wivu kidogo.Iwapo kupaka rangi kutafanywa inavyotakiwa,kutaweza badilisha maisha ya familia yako yote.Unaweza ukahisi ni furaha gani utakua nayo kwa kuingia kwenye nyumba yako ambayo inaonekana kuwa mpya,tena iking'ara kuashiria maisha mapya. Fikiria jinsi utakavyojivunia kuwepo ndani ya nyumba hii, nyumba ambayo utapenda kuwaalika rafiki zako ili waone maajabu ambayo wewe na rangi mmeyafanya.

Kitabu hiki kina misingi yote unayo hitaji kuhusu upakaji wa rangi,nini cha kununua,nini cha kufanya,jinsi ya kupaka rangi, vifaa vya kutumia,mipangilio ya rangi n.k tutafanya mipangilio yote hiyo hatua kwa hatua,na mwisho utakua mtaalamu. Pia utajionea jinsi kupaka rangi kama inavyotakiwa kulivyo rahisi na juu ya yote utapata matokeo mazuri mno.

## JINSI YA KUCHAGUA RANGI SAHIHI.

Kumbuka kwamba rangi za daraja la juu za Goldstar hukupa maisha marefu zaidi na gharama zake ni nafuu.Kuchagua rangi ni rahisi na ifahamike pia kuna makundi matatu ya rangi




1.Rangi ya mwanzo-'primer"
2.Rangi ya kati -'undercoat'
3.Rangi ya mwisho – 'top coat

Mtiririko wa makundi ya rangi hapo juu huunda kitu kiitwacho mfumo wa rangi.Ni vema ifahamike kwamba fundi anayetambua umuhimu wa mifumo ya rangi kama ilivyoainishwa hapo juu huwa na mafanikio kwa kuwa kazi yake itakuwa na ubora wa juu.

Ni vema fundi akafahamu kwa ufupi maana za makundi ya rangi kama ifuatavyo.
1.Rangi ya mwanzo (primer) -'primer'hutumika kama rangi ya mwanzo katika maeneo mbalimbali, na ifahamike kuwa kila eneo linahitaji rangi ya mwanzo ya aina yake.mfano chuma,mbao,ukuta,chip board n.k.

2.Rangi ya kati (under coat) -rangi hizi hutumika baada ya primer.Zina uwezo mkubwa wa kufunika na hivyo kufanya eneo liwe zuri tayari kupokea rangi ya mwisho (top coat). Ifahamike kuwa si kila eneo ni lazima lipakwe kundi la rangi liitwalo undercoat. Mfano wa maeneo ambayo mara nyingi 'undercoat' hutumika ni vyombo vya usafiri wa baharini, vyuma vilivyo katika ukanda wa bahari n.k

3.Rangi ya mwisho (top coat) – hupakwa juu ya rangi ya kati (under coat).Rangi ya mwisho hupakwa

kwa ajili ya kupendezesha eneo husika na kutoa muonekano uliokusudiwa. Ifahamike kuwa si lazima rangi zote za mwisho zipakwe juu ya undercoat.  Kwa mfano - Mfumo wa upakaji rangi kwenye nyumba huonyesha matumizi makubwa ya primers, fillers na rangi ya mwisho.

Angalizo:Ni budi ifahamike kwamba kitu cha msingi cha kuzingatia unapochagua rangi ni kuepuka RANGI ZA BEI NAFUU. Ni vema ukachagua rangi zenye ubora zaidi kama vile Goldstar Wash-n-Wear silk, wash n wear silk matt, Homeguard, Coastguard, Duratex, Duratough na nyingine nyingi. Usisite kuonana na timu ya ufundi ya Goldstar kwa ushauri zaidi unapotaka kuchagua ubora wa rangi.

## JINSI YA KUPAKA RANGI NA VIFAA VYA KUTUMIA.

1) Kila mara kabla ya kufanya chochote, soma maelezo yaliyoandikwa pembeni mwa kopo.Mara baada ya kufungua kopo, koroga vizuri kupata rangi inayofahamika.Kipande safi cha mbao kinaweza kutumika.Koroga vizuri mpaka rangi ambayo huende ilikua imeganda chini ya kopo iweze kuyeyuka vizuri kabisa.



2) Unapopaka rangi ndani unashauriwa kuanza na "ceiling" la sivyo unaweza kuharibu rangi yako ambayo umeshaipaka kwenye kuta. Kama unafanya kazi kwenye ukuta na unatumia mkono wa kulia,anza kupaka kona ya juu ya upande wa kushoto. Paka kwa mistari yenye upana usiozidi mita moja kutoka kwenye"ceiling" kuelekea chini ya sakafu. Kama unafanya kazi kutumia mkono wa  kushoto, unashauriwa kupaka rangi kuanzia kona ya juu ya upande wa kulia na kushuka chini ya sakafu. Kama unapaka mstari mrefu katika eneo kubwa, kuwa mwangalifu yakuwa mstari wa kwanza usiwe umekauka kabla ya kuunganisha na mstari mwingine.Usipofuata hilo basi sehemu ya muungano itaonekana.



3) Unapopaka rangi kwa nje anza juu kwenda chini.kama uko juu ya ngazi,piga rangi eneo kubwa kadri uwezavyo.



4) Kama unatumia brashi usitumbukize nywele zote za brashi ndani ya rangi, tumbukiza theluthi moja tu ya nywele za brashi. Fanya hivyo kwa mara ya kwanza polepole kwa kuwa utaruhusu brashi kunyonya rangi.Unapotoa brashi nje ya rangi,futa brashi au ncha  za nywele za brashi kwenye ukingo wa mdomo wa kopo ili kusambaza rangi sawa sawa kwenye nywele za brashi na kuondoa mapovu yaliyosababishwa na hewa.Tumia brashi kupaka rangi kwa mielekeo angalau miwili tofauti ili kupata matokeo mazuri.



5) Kupaka rangi kwa kutumia "roller" ni rahisi pia ni haraka kuliko brashi. Unahitaji chombo cha kupakia  kiitwacho "tray" au ndoo safi.Tumbukiza "roller"kwenye rangi mwisho mwa "tray" au ndani ya ndoo na  chukua rangi kidogo  kidogo kwa kuzunguusha roller kwenye chombo cha kupakia rangi



ili kuhakikisha roller haichukui rangi nyingi .Roller hupaka eneo kubwa na haifanyi tofauti kubwa yoyote kwa upande au uelekeo wowote utakao pakaa, cha msingi ni kukumbuka kufanya tabaka la mwisho (final layer)kuwa sawa (evenly).Kwa rangi za maji usirudie rudie kuzungusha "roller"sehemu moja maana unaweza kusababisha mapovu. Ikiwa wakati wa kutumia roller mapovu yatapatikana hiyo ni kawaida lakini unatakiwa usiyaache yapasuke yenyewe. Unashauriwa kutumia roller isiyo na rangi nyingi ,iweke juu ya sehemu yenye mapovu kuanzia juu ya ukuta na ishushe taratibu bila ya kukandamiza na mapovu yote yatapasuka bila kuacha vidonda.

6) Ni haraka zaidi kutumia"roller"kwa eneo kubwa. usizungushe roller haraka sana kwa kuwa utarusha rangi kwenye maeneo yasiyo hitajika au utajirushia rangi. Brashi pia inaweza kutumika kwenye maeneo yenye upana mdogo mfano : kona, grills nk. Zuia rangi kuangukia maeneo yasiyohitajika kwakutumia vifaa kama masking tepu, nailoni, box, nk






7)Wakati unaendelea kupaka rangi unaweza kuona rangi ya ndani ya kopo inaanza kuwa nzito kidogo. Kama unapaka rangi ya mafuta unaweza kutumia tina kurudisha katika hali yake ya kawaida. Kuwa mwangalifu usitumie tina nyingi na hakikisha unatumia tina sahihi.

Soma maelekezo yamatumizi kwenye kopo kwa maelezo sahihi.
Unapomaliza kupaka rangi hakikisha kuwa kopo umelifunga vizuri.Ukiacha wazi utakuta rangi imekua nzito (more viscous) na kutengeneza ngozi kwa juu. "na huo ni uharibifu wa rangi nzuri"

8) Inawezekana ikawa ni vigumu kuzuia rangi kuruka kwenye maeneo mingine hivyo unashauriwa rangi iliyorukia eneo lingine ifutwe kabla haijakauka.


9) Unashauriwa kutunza vizuri brashi na roller zako na unaweza kuzitumia kwa muda mrefu zaidi.Ni vizuri na rahisi kununua roller na brashi za ubora mzuri kwa matumizi endelevu.

Usiache brashi zako kusimamia ncha kwakua zitapinda na hazita faa tena. Safisha brashi zako na roller baada ya matumizi.Kama umetumia rangi ya maji ya Goldstar safisha brashi na roller kutumia maji safi, Kama umetumia rangi ya mafuta tumia tina iliyotumika kuyeyushia / kuchanganyia rangi kusafisha brashi au roller. Baada ya kuzisafisha unashauriwa kuzining'iniza ili zikauke.Kama hutegemei kuzitumia karibuni unashauriwa kuzihifadhi brashi vizuri bila ya kupindisha ncha zake. Hairuhusiwi kuhifadhi vifaa hivyo kwenye maji.



## KIASI CHA RANGI CHA KUNUNUA

Hakuna njia sahihi kabisa ya kujua kiasi kamili cha rangi cha kununua.Tutakupa uelekeo wa jinsi ya kukadiria hasa unapofanya kazi kwenye maeneo makubwa kama kuta na "ceilling".Inachukiza unapoanza kupiga rangi ukuta na ceilling na kujikuta umemaliza rangi kabla ya kazi au kujikuta




umenunua rangi nyingi zaidi.Mara kwa mara unashauriwa kuwa na kiasi cha kutosha cha rangi iwe kwa koti moja au mbili. Ufuatao ni mfano wa jinsi ya kukadiria kiasi cha rangi cha kutumia.

Tafuta kiasi utakachohitaji kupaka chumba au ceilling;Mfano:Chumba chenye upana wa mita 3 (futi 10)urefu wa mita 4.6 (futi 15) na kimo cha mita 2.7 (futi 9) tafuta kiasi cha rangi kitakachohitajika..




Kupata jumla ya eneo,jumlisha upana 3m na urefu 4.6 ambayo itakupa 7.6m zidisha kwa 2 ambayo itakupa 15.2m kwa hiyo jumla ya eneo itakuwa sawa 15.2m*2.7m (kimo) =41.04 mita za mraba. Kwa kuwa eneo linafahamika basi kiasi cha rangi yoyote kitakachohitajika ni rahisi kujulikana.

Mfano. a) Ikiwa rangi ya wash n wear ina uwezo wa kupaka mita za mraba 12 kwa koti moja,

HIVYO KIASI CHA RANGI KITAKACHOHITAJIKA KWA KOTI MBILI =

JUMLA YA ENEO x KOTI MBILI
ENEO AMBALO RANGI UFUNIKA KWA KOTI MOJA.

41.04 x 2 / 12= 6.84ltrs

b) Tafuta rangi itakayohitajika kupaka "ceilling.". kwa kuwa urefu =4.6m na upana = 3m

Eneo = urefu*upana
= 4.6m*3m
Jumla ya eneo = 13.8mita za mraba

Kwa hiyo kiasi cha rangi kitakachohitajika cha rangi ya Homeguard kwa koti mbili
=JUMLA YA ENEO x 2 ( kwa koti mbili)
ENEO AMBALO RANGI HUFUNIKA KWA KOTI MOJA

Kumbuka rangi ya homeguard hupaka mita za mraba 10 kwa koti moja, Kwa hiyo kiasi cha rangi kitakachohitajika = 13.8 x 2 / 10 = 2. 7 litres

NB/

1. Koti mbili za rangi inayohitajika zinashauriwa kupakwa juu ya prima husika mfano kwa ceilling ya zege na ukuta, tumia prima iitwayo Goldstar Alkai resisting primer sealer / Goldstar Alkali resisting masonry primer . Kwa ceilling za gypsum board, chipboards etc.. tumia prima iitwayo Goldstar Gypsum board primer.
2. Kuta zilizofanyiwa skimming kwa ndani na nje tumia primer iitwayo Goldstar star binder
3. Kwa kuta za ndani pekee tumia prima iitwayo Acrylic primer sealer.

## UCHAGUAJI WA SAMPULI ZA RANGI: (SHADE).

Siku hizi kuna sampuli za rangi nyingi sana (shade) kiasi kwamba kuchagua rangi iliyo sahihi inaweza kuwa vigumu mno.Lakini inaweza kuwa si tatizo kama utapanga kazi yako mapema.Kuna vitu vichache vinavyoweza kurahisisha uchaguzi wako. Mfano: unaweza kutazama rangi ya pazia za vyumba vya nyumba yako, tiles za vyumba vyako, samani za vyumba vyako.. Hii inaweza kukuongoza katika uchaguzi wa sampuli za rangi ya kupaka kuta zako. Sampuli ya rangi (shade) ni kitu muhimu sana katika kupendezesha nyumba yako.Ni vizuri familia nzima ikahusishwa katika kufanya uchaguzi wa sampuli za rangi (shade). Kama wote mtakubaliana katika chaguo lililofanyika, nidhahiri kila mmoja wenu atakuwa na furaha.Watengenezaji wa rangi za Goldstar hutoa kitabu cha sampuli za rangi "colour chart"bila gharama yoyote.Hii itakurahisishia sana katika kuchagua sampuli za rangi unazohitaji.



Vifuatavyo ni vidokezo vidogo kwenye kufanya mpangilio wa rangi,

Kama chumba ni kidogo,unashuriwa kuchagua rangi nyepesi (light colours).Sampuli za rangi hizi zitafanya chumba kiwe na nuru na pia mwanga wa kuridhisha machoni kwa kutazama.Siku hizi watu wengi hutumia sampuli za rangi (shade) tofauti kupaka kuta tofauti na hiyo huonekana kuvutia mno.

Sampuli ya rangi nyepesi (light colour) hufanya chumba kidogo kionekane kikubwa kuliko kilivyo. Sampuli za rangi nzito (dark colour) hufanya chumba kikubwa kionekane kidogo kuliko kilivyo .Hapa pia mchanganyiko wa rangi huonekana vizuri mno.Mfano vyumba vyenye joto huweza kufanya kuwa baridi kwa rangi zenye kionjo cha blue na kijani.Jikoni kwa kawaida huitajika sampuli za rangi ambazo ni nyepesi (light colour) na baridi (cool colour).

Sehemu ambazo kuta huchafuka sana,ni vizuri zaidi kutumia rangi ambayo ni rahisi kusafisha.
Mfano wa maeneo hayo ni jiko na bafu.Rangi za mafuta za Goldstar hupendekezwa katika maeneo hayo.Rangi zilizo bora za Goldstar kama PVA-Acrylic wash-n-wear silk n.k.hutumika zaidi katika "bed room", "Living room", "dining room" n.k.

NB/ 1. Kwa sampuli za rangi ya nje fundi anatakiwa awe na uelewa wa kutosha juu ya sampuli za rangi zinazopauka na zisizopauka. Wataalamu wako wa kiwanda cha rangi cha Goldstar wanaweza kukusaidia katika utambuzi huo.

## NINI CHA KUFANYA KABLA YA KUANZA KUPAKA RANGI.

Kitu cha msingi kabisa ambacho hupaswi kabisa kukifanya ni kujaribu kufunika maeneo machafu kwa kutumia rangi bora.Ukifanya hivyo utakua umepoteza muda wako na fedha bure.



1. KUTA

Kabla ya kuanza kupaka rangi kwenye kuta unatakiwa kuhakikisha kama zimekauka.Kama hazijakauka rangi itamenyeka (peel off). Mabomba yanayovuja karibu ya msingi na katikati ya kuta za nyumba yanaweza kuwa sababu ya unyevuunyevu kwenye kuta.

Tatizo la rangi kutokana na unyevu linaweza kurekebishwa, lakini lazima kwanza kujua chanzo cha unyevu. Kama utashindwa kujua basi muone mjenzi wa jengo hilo akusaidie..

2. Jambo la muhimu lakufanya ni kuhakikisha kwamba kuta hazina oil, grease, vumbi, rangi za zamani zinazobanduka, kuta zenye ukungu ( fungas) na kuta zenye asili ya chumvi nk. Kuta zote za zamani lazima zisafishwe vizuri. Ondoa rangi zinazomenyeka kwa kutumia "scriper" au "brush" ya chuma. Hakikisha kuta zenye oil na grees zinasafishwa vizuri kwa kutumia sabuni ya maji. Hakikisha kuta zenye fangas zinatibiwa kwa kutumia dawa ya kuua fangas iitwayo algae kill, kuta zenye asili ya chumvi chumvi ni lazima zitibiwe na undercoat iitwayo HB damp sealer. Vyote hivyo hutengenezwa na kiwanda cha rangi cha Goldstar. Kupaka rangi kwenye maeneo yenye matatizo bila ya kuyatibu ni kujitafutia matatizo zaidi.





Koti moja ya "primer"ya Goldstar iitwayo "starbinder"lazima ipakwe kwenye eneo lolote lenye plasta au kuta zilizochoka na vumbi kabla ya kupaka rangi ya mwisho.

3. Lingine la msingi nikuangalia kuta kama zinanyufa (cracks), nyufa ndogondogo au nyembama zijulikanazo kama (hairline cracks) si vigumu kudhibiti. Tumia stucco putty interior au stucco putty exterior. Ikiwa ufa utakuwa mkubwa unatakiwa kufikiria utatuzi maalumu kama kufanya plaster upya.



## KUPAKA RANGI MBAO ZILIZO NJE YA NYUMBA.

Katika kuamua upakaji wa rangi wa mbao za nje inalazimika kuwa mwangalifu kwa kua jua kali na mvua husababisha mbao kuharibika kabisa ikiwa rangi inayoweza kupambana na hali hiyo hazitatumika. Mfano. Goldseal, gypsum primer, Eggshell enamel, Duramatt enamel, Timbatex nk

### (a) FRAME ZA MADIRISHA ZA MBAO ZA NJE

Siku hizi fremu za mbao zimeshaanza kuachwa kutumika polepole na fremu za chuma kuchukua nafasi yake,lakini sehemu ambazo mbao zinatumika unapaswa kuziandaa vizuri kabla ya kupakwa rangi au Varnish. Zichunguze vizuri fremu zako za mbao, hakikisha ziko kwenye hali nzuri.; Hakikisha fremu ni safi na kavu. Fremu zilizo katika hali nzuri hupakwa rangi au varnish kwa matayarisho madogo mno.(light sanding down). Unaweza kutumia varnish bora za goldstar mfano Goldseal, Indusrial PU clear, Timbatex nk Au unaweza kutumia rangi bora za mafuta za Goldstar.Kama Eggshell enamel,Duramatt enamel, nk. Fremu za zamani ambazo rangi imeanza kubanduka unashauriwa kuiondoa yote kwa kutumia dawa ya kuondolea rangi iitwayo "PAINT REMOVER"
-Baada ya kuondoa rangi yako kwa kutumia "paints remover"unashauriwa kusafisha mbao kwa kutumia "GP Thinner" ( Solvent)
-Baada ya kusafisha na kuacha ikauke, paka primer za mbao za Goldstar ziitwayo "pink wood primer au Gypsum board primer au Duraseal GP undercoat.
-Baada ya primer kukauka kwa muda wa masaa 18, utaendelea kupaka rangi za mwisho za Goldstar ( top coats) zijulikanazo kwa jina la Eggshell enamel, Duramatt enamel n.k.

Lakini ikiwa mbao hizo zinahitaji kupakwa varnish ya nje unashauriwa kupaka Goldseal, Timbatex industrial PU koti mbili hadi tatu moja kwa moja kwenye mbao.

### ONYO

Unapotumia "paints remover"kuwa makini kwani inavionjo ambavyo vinaweza kukuathiri..
-Fungua mfuniko kwa uangalifu na polepole kuruhusu mgandamizo wa hewa ndani ya kopo kutoweka, Weka mbali na watoto pia epusha ngozi na macho yako. Unashauriwa kuvaaa vifaa vya kujikinga ili kuwa na uhakika za kuepuka athari za bidhaa hii.

### (b)MILANGO YA NJE

Milango ya nje ya mbao huhitaji uangalizi maalumu ili kuilinda kutokana na jua kali na mvua. Wauzaji wa rangi za Goldstar wanaweza kukushauri nini cha kutumia.

### (c) ROOF BOARDS / FISCIA BOARD

-Boards mpya za mbao lazima zipigwe msasa.
-Baada ya msasa unashauriwa kupaka primer ya mbao iitwayo Gypsum board primer, hakikisha kona za juu na maeneo ya nyuma yanashughulikiwa bila kusahaulika.



-Kwa sehemu ambazo zilishapakwa rangi na bado ziko katika hali nzuri unashauriwa kupiga msasa laini, pangusa vumbi na kisha paka rangi za mafuta za Goldstar mfano Eggsheel enamel, Duramatt enamel.
-Ikiwa rangi iliyopigwa inapanduka inashauriwa kuitoa kwa kutumia PAINT REMOVER na SCRIPPER kisha unaweza kuendelea na hatua zinazofuata.

## KUPAKA RANGI MBAO ZA NDANI

### "WOODEN FURNITURE "

Matayarisho yanayohitajika unapotaka kupaka rangi "furniture"ni sawa na fremu za dirisha.

### MILANGO YA NDANI YA MBAO NA FREMU ZAKE

Milango na fremu zinaweza kupakwa rangi kama ilivyo katika mbao za nje cha msingi ni kukumbuka mambo ya msingi yafuatayo;
(a)Eneo lazima liwe safi kwa kupiga msasa na kufuta vumbi. Mbao lazima ziwe zimekauka



(b)Baada ya msasa unaweza kupiga primer za mbao kama zilivyoainishwa kwenye kushughulikia mbao za nje ya nyumba," na mwisho rangi ya mafuta. Hatua hizo huweza kufuatwa pale tu milango na fremu zinapokuwa katika hali nzuri.

(c)Kama rangi iliyopigwa inabanduka unashauriwa kuitoa kwa kutumia "PAINTS REMOVER, SCRIPER" na msasa.

(d)Baada ya kuitoa rangi inayobanduka na kusafisha vizuri unaweza kupaka primer ya mbao ya Goldstar iitwayo gypsum board primer na kufuatiwa na rangi mwisho ya mafuta mfano Eggshell enamel au Duramatt enamel.
e) Ilkiwa utaamua kufanya umaliziaji kwa kutumia varnishi , kumbuka Goldstar wanakupa bidhaa zao za Turbobright, Sanding sealer, Nc lacquer au varnish ya kawaida.

# KUPAKA RANGI CHUMA.

## (a) FREMU ZA MADIRISHA ZA CHUMA.

1. Chuma cha zamani



-Fremu za chuma nyingi zinatengenezwa kutokana na chuma kiitwacho "steel". kama fremu yako imepata kutu au rangi iliyopakwa kubanduka lazima zisafishwe mpaka chuma halisi kionekane. Jinsi ya kufanya nikupiga msasa laini kuondoa kutu. Lakini unaweza kutumia bidhaa ya Goldstar iitwayo Rust convetor il kupambana na kutu inayo onekana kwa wingi kabla ya kuendelea na maelekezo yanayofuata.
-Ukishafanya hivyo unaweza kupaka primer ya Goldstar za hali ya juu ziitwayo"Zinc phosphate, Etch primer, au Epoxy primer koti moja kwa ajili ya kuzuia kutu,kisha unaweza kupaka koti mbili za rangi bora za mwisho za Goldstar kama 2k marine paint n.k

## 'GUTTERS" NA MABOMBA YA ARDHINI.



Gutters na mabomba ya ardhini kwa kawaida yanatengenezwa kwa chuma kiitwacho GALVANIZED IRON" Mara nyingine huweza kutengenezwa kwa kutumia ASBESTOS CEMENT au PLASTICS. Kama ni Galvanized iron au Plastics,utahitaji kupaka primer ya Goldstar iitwayo ETCH PRIMER ili kuwezesha rangi kushika vizuri na baadae kupaka rangi za mwisho za Epoxy enamel au Bituminous black kwa mabomba ya ardhini, na unashauriwa kutumia rangi ya mwisho ya Goldstar iitwayo 2k industrial pu au rangi za mafuta za goldstar kama Hi gloss enamel, Duramatt enamel, Eggshell enamel etc kwa ajili ya Gutters.

Kama rangi ya zamani inabanduka,unashauliwa kuitoa yote na kuanza upya. Unaweza kutoa rangi yote kwa kutumia paint remover, lakini kama rangi ya zamani bado ni nzuri,unashauriwa kupiga msasa laini na kupaka rangi ya mafuta. Ikiwa Gutters na mabomba ni ya Asbestors rangi ya maji ya Goldstar kama vile PVA ACRRYLIC – HOMEGUARD, WASH N WEAR au WEATHERGURD,inaweza kutumika moja kwa moja. Kwa ASBESTOS mpya unashauriwa kupaka koti mbili hadi tatu. Ikiwa gutters na mabomba ya ardhini ni ya galvanised iron na plastics, unashaurie kutumia primer ya Goldstar iitwayo Etch primer kabla ya kuendelea na mpangilio wa rangi za mwisho kama zilivvo ainishwa hapo juu.

-Si primer au rangi zote zinafaa kwa ajili ya Gultter na mabomba yanayotumika kukinga maji ya kunywa kutoka kwenye paa.Kama unaitaji kukinga maji kutoka kwenye paa,unashauriwa kuwaona wauzaji wa wa rangi za Goldstar kwa ushauri zaidi.

### MILANGO YA GEREJI NA MAGETI

Milango mingi ya gereji imetengenezwa kwa kutumia chuma cha aina "STEEL" Kupaka rangi milango hii unashauriwa kutumia rangi zenye ubora mkubwa, zinazoiweza kupambana ma mazingira maguma ya oil na grisi bila kuharibika. Hivyo ili kupata matokeo mazur kwa milango ya gereji iliyojengwa kwa chuma aina ya steel unatakiwa kupaka primer ya Goldstar iitwayo Epoxy primer, na kisha malizia kwa rangi ya mwisho ya Goldstar iitwayo Industrial polyurethane, Kwa mageti yaliyotengenezwa kwa chuma cha galvanised unashauriwa kupaka primer ya Goldstar iitwayo Etch primer na kisha malizia na rangi ya mwisho iitwayo Industrial Polyurethane.

## PAA ZA GALVANISED IRON NA ASBESTOS

Hii ni kazi kubwa ambayo inahitaji rangi nyingi. Kwasababu hiyo na muda unaohitajika ni muhimu kuandaa paa lako vizuri kabla ya kupaka rangi."Safisha vizuri paa lako na hakikisha limekauka vizuri kabla ya kupaka rangi.



- Ikiwa paa limetengenezwa kwa bati, paka primer ya Goldstar iitwayo "Etch primer"na kisha paka koti mbili za rangi ya Goldstar ya paa iitwayo Roofguard acrylic PVA.

-Kama paa lako lilisha pakwa rangi,na rangi ilisha anza kubanduka unatakiwa uchune yote na kuanza upya.

-Ukishafanya hivyo paka koti moja ya Etch primer ikifuatiwa na koti mbili za rangi ya paa.



-Kama rangi iliyopakwa bado ipo katika hali nzuri,unashauriwa kusafisha paa na kupaka koti mbili za rangi ya paa moja kwa moja.

-Kama una paa la zamani halijapakwa rangi na lina alama ya kutu paka rangi ya kutibu kutu yaani "Rust Convetor" kwenye maeneo yenye kutu na kisha acha kwa muda wa masaa 18, kisha paka Etch primer koti moja ikifuatiwa na rangi ya paa iitwayo Roofguard PVA. Paa linavuja linaweza kulekebishwa kwa kutumia "Roofing compound" kabla ya kupaka rangi.

-Kama unapaa la Asbestos au roof tiles upakaji wa rangi utauona kuwa rahisi sana,na si gharama sana kiutendaji.

-Kwanza unatakiwa kulisafisha paa lako vizuri kuondoa uchafu na vumbi lililoganda juu ya paa. Paa likishakauka unaweza kupaka koti moja ya rangi ya bati iitwayo "ROOFGUARD ACRYLIC" PVA koti mbili. Koti ya pili ni baada ya koti ya kwanza kukauka kwa masaa 4.

Nimatumaini yetu kitabu hiki kimekupa mwanga wa safari yako ya kutaka kuwa fundi rangi bora. Timu ya ufundi ya Goldstar inakuahidi kwamba itakuwa bega kwa bega nawe ili kuhakikisha malengo yako yanatimia.

-Kwa kumalizia tunapenda kukukumbusha kwamba Goldstar ina aina mbalimbali za rangi kwa maeneo tofauti kama ifuatavyo:

**1. RANGI ZA MAJI**
- G.S AQUA GOLD
- G.S HI-COVER EMULSION
- G.S CONTRACTOR EMULSION
- G.S HOMEGUARD INTERIOR / EXTERIOR
- G.S WEATHER GUARD
- G.S WASH N WEAR MATT
- G.S WASH N WEAR SILK

**2. RANGI YA KULAINISHA KUTA**
- G.S STUCCO PUTTY INTERIOR
- G.S STUCCO PUTTY EXTERIOR

**3. RANGI ZA MAFUTA**
- G.S HI-GLOSS ENAMEL
- G.S EGGSHELL ENAMEL
- G.S COAST GUARD MASONRY PAINT
- G.S SUPER HI GLOSS ENAMEL
- G.S DURAMATT ENAMEL

**4. RANGI ZA MAPAA (ROOF PAINT)**
- G.S ROOF PAINTS GREEN/RED
- G.S ROOFGUARD ACRYLIC PVA (VARIOUS COLOURS)

**5. RANGI ZA SAKAFU.**
- G.S FLOOR PAINTS GREEN/RED
- G.S PVA FLOOR COATING GREEN/RED
- G.S INDUSTRIAL POLYURETHANE COATING
- G.S INDUSTRIAL EPOXY ENAMEL

**6. VARNISHES**
- G.S TURBOBRIGHT GLOSS / EGGSHELL/ MATT CLEAR
- G.S HI-CHEM ENAMEL EPOXY CLEAR
- G.S INDUSTRIAL POLYURETHANE GLOSS / EGGSHELL / MATT CLEAR
- G.S GOLDSEAL SHADES AS PER SHADECARD
- G.S VARNISH – GLOSS / EGGSHELL / MATT CLEAR
- G.S WOOD STAIN
- G.S NC STAIN
- G.S SANDING SEALER
- G.S. TIMBAPRESERVATIVE CLEAR / TINTS
- G.S NC LAQUER GLOSS/EGGSHELL/ MATT CLEAR
- G.S. VARNISH ECONOMY GLOSS CLEAR
- G.S TIMBAFLEX CLEAR AND TINTS

**7. VARNISH ZA MBAO AMBAZO HAZIKO JUANI NA KWENYE MVUA.**
- G.S TURBOBRIGT GLOSS / EGGSHELL/ MATT CLEAR
- G.S VANISH GLOSS / EGGSHELL / MATT CLEAR
- G.S NC LAQUER GLOSS / EGGSHELL / MATT

- G.S VARNISH ECONOMY GLOSS CLEAR

**8. VARNISH ZA MBAO AMBAZO ZIPO JUANI NA KWENYE MVUA.**

- G.S INDUSTRIAL POLYURETHANE CLEAR
- G.S GOLDSEAL AND ITS COLOURS
- G.S TIMBATEK
- G.S TIMBA PRESERVERTIVE

**9. VANISH ZA MAJI**

G.S TIMBAFLEX
G.S GOLDSEAL

**10. RANGI ZA BARABARA**

G.S ROADMARKING WHITE/YELLOW

**11. RANGI ZA BOILER NA CHIMNEYS**

G.S HEAT RESISTING ALUMINIUM

**12. RANGI ZA VIWANJA VYA TENNIS**

- G.S TENNIS COURT PAINT (ORDINARY)
- G.S HARD TOUGH (LUXURY)

**13. RANGI ZA MWANZO (PRIMER) KWENYE CHUMA**

- G.S RED OXIDE PRIMER.
- G.S ZINC PHOSPHATE PRIMER.
- G.S ETCH PRIMER
- G.S HB EPOXY PRIMER (MARINE PRIMER)
- G.S 2K PRIMER
- G.S NC AUTO GREY PRIMER
- G.S NC MATT BLACK SPECIAL

**14. PRAIMA MAALUMU YA NJE NA NDANI KWA KUTA ZENYE TABIA YA CHUMVICHUMVI**

- G.S HB DAMP SEALER

**15. RANGI MAALUM YA UKUTA KWA MAENEO YALIYO KARIBU NA BAHARI**

- G.S DURACOTE MASONRY PAINT

**16. RANGI YA KUCHUNIA RANGI NYINGINE**

- G.S PAINT REMOVER (HYDROSOLVER)

**17. PRAIMA YA KUPAKA KUTA ZA ZAMANI ZENYE VUMBI**

- G.S STAR BINDER

**18. PRAIMA KUPAKA KUTA ZILIZOJAZWA NA STUCCO KWA NDANI**

- G.S ACRYLIC PRIMER

**18. RANGI/PRIMER KUPAKA KUTA ZILIZOJAZWA NA STUCCO PUTTY, WHITE CEMENT AU JK WALL PUTTY**

- G.S STAR BINDER / ECOBOND

**19. RANGI ZA TEXITURE:**

- G.S DURAPLAST FINE ( For interior use)
- G.S DURAPLAST COURSE ( For exterior / interior use )
- G.S DURASTONE ( For interior / exterior use )
- G.S DURASTUCCO ( For interior / exterior use ) - 2pack
- G.S DURATOUGH ( For interior / exterior use )
- G.S DURA SAND ( For interior / exterior use)
- G.S DURA DESIGN ( For interior / exterior ) - 2pack
- G.S DURA ANTIQUA ( For interior / exterior)

**20 . RANGI NYINGINE MAALUMU NI**

- G.S ALGAE KILL
- G.S WATER REPELLENT SILICONE SOLUTION
- G.S BITUMINOUS PAINT BLACK
- G.S BLACKBOARD AND GREENBOARD PAINTS
- G.S GYPSUM BOARD PRIMER
- G..S DURASEAL GP UNDERCOAT
- G.S SPARKLING ALUMINIUM
- G.S RUST CONVETOR
- G.S ALKALI RESISTING MASONRY PRIMER ( solvent base)

Goldstar ina rangi maalumu nyingi kwa maeneo mbalimbali, haiwezekani kutaja yote lakini kwa uchache ni

-Rangi za meli/boti

-Rangi za matanki ya kuifadhia petrol na dizeli.

-Rangi za kupaka swimming pool n.k

Ni mengi zaidi ya yaliyotajwa kwenye kitabu hiki ambayo Goldstar inaweza kufanya katika ulimwengu wa rangi.

Tafadhali usisite kuwasiliana na timu ya ufundi ya Goldstar kwa mahitaji yoko yote ya rangi na ushauri.

*Kimetolewa kwa hisani ya kiwanda*
*cha rangi cha Goldstar*

*Supplied with the compliments of*
*The manufacturers of Goldstar paints Tanzania Ltd.*


## Headquarters & Factory

**106, Mwakalinga Street, Chang'ombe, P.O.Box. 909, Dar es Salaam, Tanzania.**
**T: +255 22 2865222 / 2862933 / 2862964 / 2861677 / 286 0670**
**M: HQ: +255 748 500001 / +255 754 788366 / 754 788367**
**E: info@goldstarpaints.co.tz : www.goldstarpaints.co.tz**
**f: GoldstarTZ : GoldstarPaintsTZ : GoldstarPaintsTZ**


**An ISO 9001:2015 Certified Organization**

## Branches

**Nkuruma:**
**+255 748 500002**

**Arusha:**
**+255 748 500003**

**Moshi:**
**+255 748 500004**

**Mbeya:**
**+255 748 500005**

**Mwanza:**
**+255 748 500006**

**Singida:**
**+255 748 500007**

**Dodoma:**
**+255 748 500008**

**Tabora:**
**+255 748 500009**

**Kigoma:**
**+255 748 500010**